

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA KUMI NA MOJA**

**20 APRILI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA KUMI NA MOJA – TAREHE 20 APRILI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**136. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI  
(CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya Kwamtoro - Sanzawa hadi Mpendo katika Wilaya ya Chemba.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**137. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI  
(NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini Wanufaika wa TASAF wasilipwe mkononi badala ya kupewa kwa njia ya simu na benki.

**138. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH  
SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Serikali itafufua upya Tume ya Taifa ya Mipango.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**139. MHESHIMIWA SHAMSIA AZIZI MTAMBA  
(MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iyari hadi Mkunwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

**140. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHAN SIMA (SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya mchepuko kutoka Kisaki – Unyamikumbi - Unyambwa hadi Mtipa.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**141. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga Minara ya simu katika Kata za Kikolo, Mbangamao, Kitanda na Kagugu - Mbinga.

**WIZARA YA NISHATI:**

**142. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini umeme wa REA utafika katika Kijiji cha Ikombe - Kyela.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **143. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini mabwawa na mifereji itajengwa ili kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji na kupunguza athari za mvua Kilimanjaro.

## **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

### **144. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kuna utafiti uliofanywa na Serikali kujua sababu za uwepo wa Watoto wa Mitaani.



#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
20 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**